

**HOTUBA YA MKURUGENZI MTENDAJI AKIHITIMISHA MAFUNZO YA
MFUMO WA PLANREP TAREHE 16/10/2017**

Ndugu Washiriki; Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Washiriki wote (*Wakuu wa Idara na Vitengo*), Wakufunzi (wakiongozwa na DPLO), Mwenyekiti wa Mafunzo na maafisa wote kwa namna ya pekee mmeweza kufanikisha mafunzo haya kwa siku tatu. Natambua uzalendo na umoja mliounesha hata mkaweza kutumia siku za jumamosi na jumapili ambazo kimsingi mlipaswa kupumzika na wengine kuabudu; Mungu awabariki sana na kuwazidishia zaidi.

Ndugu Washiriki, Kabla sijayafunga rasmi mafunzo haya nina mambo MATATU niwaelekeze:-

Moja; Japokuwa leo hii tumemaliza mafunzo haya haitoshi kuridhika kwani mifumo hii ya Kompyuta huhitaji mazoezi ya kutosha ili kujiimarisha katika kila vipengele ambavyo tumejifunza. Hivyo niwaombe kila mshiriki mmoja mmoja kuendelea kufanya mazoezi binafsi na kwa ujumla wetu tutapanga utaratibu mzuri ambao utatupa fursa ya kuendelea kujinoa angalau hata kwa masaa matano katika wiki.

Pili; Niwaombe kuanzia sasa wakuu wa Idara na Vitengo kuanza kutoa na kukusanya mapendekezo yanayoendana na dira ya Serikali ya Awamu ya Tano kwa maana ya mwelekeo mzima wa TANZANIA YA

VIWANDA tuweze kuhuisha (update) Strategic Plan, tutajadili katika vikao vyetu vya CMT na hatimaye mapendekezo hayo yataenda katika kamati kwa ajili ya approval. Tukumbuke kuwa mipango yetu mingi ilipangwa wakati wa kipindi cha Serikali ya awamu ya NNE hivyo hatuna budi kulitekeleza hili kwa weledi mkubwa. Vilevile Action Plan ziboreshwe na tujiwekee mipango mahususi, tunayoimudu kuitekeleza, kwa wakati uliopangwa na kwa kiwango cha juu kabisa (100%).

Tatu; Mfumo huu unaenda kuweka uwazi mkubwa katika shughuli zote za upangaji mipango na bajeti zetu (complete planning cycle) hivyo sasa kila hatua tutakayoifanya inaenda kuonekana (tutakuwa exposed), umakini na ustadi mkubwa unahitajika katika Mfumo huu wa PlanRep.

Mwisho; Naamini katika weledi mlionao na ninaamini kuwa tukiamua kwa dhati tunaweza sina mashaka juu ya hilo. Kama tulivyoweza kufanya vizuri kwenye maeneo mengine ya kiutendaji ili Halmashauri ya Kaliua iendelee kuwa miongoni mwa Halmashauri zinazofanya vizuri nchini.

BAADA YA KUSEMA HAYA: SASA NATAMKA RASMI KUWA MAFUNZO NIMEYAFUNGA.

---ASANTENI SANA---